SHEIKH MASH-HUR HASAN AL-SALMÂN [HAFIDHWAHULLÂH]

KUWAHUSU WENYE KUDAI YAKWAMBA SHEIKH ‘ALI HASAN AL-HALABI AL-ATHARI NI MURJI’AH[1]

SUALI:

Wasemaje kuwahusu watu wanaodai yakwamba”Sheikh ‘Ali al-Halabi ni miongoni mwa Murji’ah, tena yeye peke yake, na wala sio Mashekhe wengine (wa ki-Salafi kutoka Jordan)?”

JAWABU:

Wallâhi, mimi sijui (kuhusu madai kama hayo)!? Ikiwa Sheikh ‘Ali (*hafidhwahullâh*) ni Murji’, basi hapana budi na Sheikh al-Albâni naye atakuwa ni Murji’, kama ambavyo na wanafunzi wake nao pia watakuwa kama hivyo! Sheikh ‘Ali (*hafidhwahullâh*) hana ‘aqîdah yake maalum[2], Sheikh ‘Ali anakiri na kuthibitisha ‘aqîdah ya Ahlus Sunnah na anamtetea Sheikh wetu katika baadhi ya mas’ala kwa undani kabisa yanayohusiana na ‘Imân na mas’ala mengine ya ki-fiqhi yanayofungmana na ‘Imân. Kwahivyo, yoyote mwenye msingi mzuri wa Usûl wa Ahlus Sunnah katika mas’ala yanayofungamana na ‘Imân, basi mtu kama huyo ni miongoni mwa Ahlus Sunnah na haifai kusemwa yakwamba mtu kama huyo ni Murji’. Lakini hatahivyo, baadhi ya watu wana wasiwasi na uharibifu ndani ya nyoyo zao kumuhusu Sheikh al-Albâni na hupotosha maneno na kusema mambo kama “Sheikh al-Albâni hamkufurishi mwenye kumtukana Allâh”, “Sheikh al-Albâni ni mgonjwa wa ki-ilimu”, “Sheikh al-Albâni ni miongoni mwa Murji’ah” *na kadhaalika*. Kwahivyo, hebu tuseme yakwamba Sheikh amekosea kwenye mas’ala, katika Usûl ya Imân, Sheikh al-Albâni anakiri na kuthibitisha ‘aqîdah ya Ahlus Sunnah na kumuhukumu mtu yakwamba yeye ni miongoni mwa Ahlus Sunnah au si miongoni mwao inategemezwa juu ya misingi ya suala lenyewe. Kisha baada ya hapo, kuna mas’ala tanzu ambayo ingawa mtu ana wasiwasi

[1] Kutoka katika muda wa Masuali/Jawabu, tarehe 7th November, 2009. Chapa asili www.mashhoor.net

[2] **NUKTA YA MFASIRI:** Hapa vilevile tunaweza kuongezea yakwamba Sheikh ‘Ali hana mfumo wake mwenyewe wa “kujitengezea na kubuni misingi ya jarh wat’ Ta’dîl”!? Mengi ya hayo yatakuja hapo mbele.

na akasema urongo dhidi ya ma-‘Ulamaa wa Waislamu huanza kujivurumizia tuhuma kubwa kubwa:

“Huyu Sheikh ni Murji’” na kisha baadae:

“Aqîdah ya Sheikh ni potofu” na baada ya hapo:

“Sheikh huyu si faqîh wala si Muhaddith” kisha:

“Sheikh huyu anafuata Manhaj ya Muta’akhirîn katika hadith na jambo hili halikubaliki” mara nyengine:

“Sheikh al-Albâni ni ZIRO na hana ajualo”!

Hili ndilo jambo watakalo! Hili ndilo jambo watakalo! Sisi hatusemi yakwamba Sheikh al-Albâni ametakasika na mapenzi yetu juu ya Sheikh wetu ni kama mapenzi ya wanafunzi wengine kwa mashekhe zao na nyoyo zetu ni kunjufu kwani sisi twampenda Sheikh wetu na twawapenda wengine pia. Tunaweza kuwa na chaguo (la ki-Fiqhi) ambalo si chaguo la sheikh wetu na dalili ni mambo yaliyotuongoza sisi kwenye rai hizo na hii ndiyo Manhaj ambayo Sheikh wetu aliyotufundisha sisi. Sisi tunamkubali Sheikhul Islâm Ibn Taymiyyah lakini kuna baadhi ya mas’ala ambayo sisi hatukubaliani naye na kuna baadhi ya mas’ala ambayo Ibn al-Qayyim hakukubaliana na Sheikhul Islâm, na kuna mas’ala ambayo ndani yake Sheikh Ibn ‘Uthaymîn hakukubaliana na Sheikhul Islâm. Hivi ndivyo ilmu ilivyo. Sisi si wa mwanzo wala wa mwisho kuhusiana na haya, hii ndiyo Manhaj ya ma-‘Ulamaa’. Mwenye kupatia hupata thawabu mara mbili haliyakuwa mwenye kukosea hupata thawabu mara moja.

Kwahivyo mas’ala ni mapana mno na nyoyo zetu hazina budi kuwa safi tusizuwe chochote na tunapaswa kukubaliana juu ya mambo ambayo waliyokubaliana nayo wale waliokuwa kabla yetu. Hii yote ni madh-hab iliyo na kina kikubwa katika historiya nasi ni wenye kuipitia njia hiyo, hii ndiyo njia ya ma’Ulamaa waliokuwa kabla yetu. Sisi hatumtukuzi Sheikh wetu, sisi hatumchukulii yeye kuwa ametakasika, lakini naapa kwa jina la Allâh, ambaye hapana mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye, sisi twajitenga na kila mwenye kuikashifu ‘aqîdah ya Sheikh wetu (al-Albâni**). Sisi twajitenga nafsi zetu kwa (ajili ya) Allâh na wao na tunawachukiya kwa ajili ya Allâh na tunawatahadharisha watu dhidi yao**[3]**.** Ikiwa wanasema yakwamba Sheikh

[3] **NUKTA YA MFASIRI:** Hii ni nukta muhimu sana kutoka kwa Sheikh kwani kuna wengi ambao kazi zao ni kujivurumizia tamko la **“Murji’ah”** kila endapo na haliyakuwa halielewi tamko hilo kama walivyolifahamu Salaf.

Hii ni naswiha muhimu kwa wale ambao, kuanzia mwishoni mwa mwaka wa 1990, walikuwa wakimtuhumu Imâm al-Albâni kwa kuwa na irjâ’ kutokamana na kumuandama kwao ki-upofu Safar al-Hawâli. Kwa hakika kuna watu fulani, wamejengewa dhana katika fahamu zao kuhusu tuhuma hii kutokana na uzito wa kusukumwa na mfano wa Safar al-Hawâli, Salmân al-‘Awdah, Abu Baseer at-Tartûsî (Sheikh bandia kutoka kusini-mashariki mwa London) na kwa kupitia kwenye midahalo ya kijinga ya hadharani yeye na Ali Tamimi. Pamoja na kuitumia *al-Muntada al-Islami* kama msingi wake ambapo ndipo alipokuwa akihudumikia. Mtu mmoja pia alianza kuwatangazia vijana yakwamba Imâm al-Albâni hakuwa akifahamu “ukweli wa imân”?!

Mambo haya yalitokana na kuwa na pupa na kundi la kusaidiana la Dr. Safar al-Hawali na Abu Baseer at-Tartûsî, na pia juu ya msimamo wa kugeuza Manhaj mara kwa mara kuliko abalishishwavyo mtoto mchanga ubinda wake! Kwa hakika, baadhi ya ushawishi wao katika mas'ala haya ulikuwa ni matokeo ya kuchanganyikiwa ki-manhaj, jambo lililoleta kudunda juu na chini kama bembea! Baadhi yao sasa hivi wametatizika na kuanzisha mfumo mpya wa kuwasukumiza vijana kwenye takfiri, mpaka wengine wakawachwa nje wakipepesuka, huku wakijaribu kubuni manhaj mpya ya vijana chipukizi!

Hivi karibuni, kumetokeza kijana mmoja, kwa jina la Zubayr Sâlim "al- 'Azzâmi", akijigamba kwenye ukumbi wa mtandao – *Islamic awakening (mwamko wa Uislamu)* – yakwamba **"ameshamtuhumu mtu mkubwa hata kuliko al-Albâni kwa kuwa na Irjâ'"!!?** Hapa alijitokeza na kudai yakwamba alikuwa na ufahamu wa kina katika mas'ala kuhusiana na 'aqîdah, jambo ambalo kwa njia moja au nyengine likamruhusu yeye kuwa na 'ilmu zaidi hata kuliko Mujaddid wa zama zetu. Amepata msukumo makhsusi wa Ghuluw na mubâlaghâ katika suala hili na kuzama ndani yake ili apate kumkanganya Muislamu wa kawaida. Jambo hili likamfanya Abû Zubayr akazidi kujitweza kwenye daraja ya chini, ambapo akailinganisha 'aqîdah ya Imâm al-Albâni na ile ya *Jahmiyyah* na *ashâ'riyyah?!* Uwoga kama huo vilevile umeshuhudiwa kwenye kuwashambulia ki-ubinafsi, ma-Salafi pasi na haki, bila ya kuwa na uso wa kuwakabili, na pia kwa tabia yake chafu ambayo asiyostahiki kuwa nayo mtu anayechukuliwa kuwa ni twâlib ul-'ilm.

Aliulizwa Imâm Ahmad bin Hanbal kumuhusu mtu asemaye "imân inapanda na kushuka" naye akajibu **"mtu huyu ame-epukana na irjâ'**, Tizama katika *al-Khallâl, as-Sunnah, vol.3; Uk.581.* Imâm Ibn al-Mubârak alimwambia Qâdhi Abî Ya'lâ, kama ilivyotajwa katika *Tabaqât ul-Hanâbilah, Vol.2; Uk.40*: **"Yoyote mwenye kusema yakwamba imân ni kutamka na kitendo na inapanda na kushuka, basi itakuwa irjâ', kuanzia mwanzo wake hadi mwisho wake, imemuacha mtu kama huyo."** Imâm al-Barbahârî pia amesema maneno kama hayo katika *Sharh as-Sunnah* Uk.132. haya ndiyo ambayo yaliyosisitizwa na ma-Imâm wa Salaf kuwa ni miongoni mwa 'aqîdah ya Salaf, na haliyakuwa baadhi ya mashekhe wa zama hizi kutokamana na Khalaf (!) wamekwenda zaidi ya hapo na wakataja viwango vyengine ambavyo visivyokuwa na dalili yoyote. Tafauti baina ya Murji'ah na Ahlus Sunnah vilevile imeelezwa na Imâm Sufyân ath-Thawrî (*rahimahullâh*), aliyesema:

> **"Sisi tunasema yakwamba Imân ni maneno na kitendo, haliyakuwa wao (murji'ah) wanasema yakwamba Imân ni maneno na wala sio kitendo. Sisi tunasema Imân inazidi na kupungua, haliyakuwa wao wanasema imân haizidi wala haipungui."**

Tizama katika *al-Îmân* (Maktaba al-Islâmiyyah), Uk.184. vilevile kutoka katika alama za Murji'ah kulingana na Salaf ni kuwa Murji'ah wanaonelea yakwamba viongozi hawafai kutwi'iwa. Angalia riwaya yenye silsila iliyo swahîh yakwamba Ahmad bin Sa'îd ar-Ribâtî amesema yakwamba 'Abdillâh bin Twâhir alimwabia yakwamba watu anaowachukia zaidi yeye ni Murji'ah kutokana na kuonelea kwao yakwamba viongozi hawafai kutwi'iwa; tizama kitabu cha Imâm as-Swâbûnî, *'Aqîdat us-Salaf wa As-hâbul Hadîth'* Uk.109. vilevile rejea kwenye riwaya ya Sufyân ath-Thawrî aliyesema: **"Mimi nitakuwaje Murji' ikiwa sionelei yakwamba upanga utumiwe (kwa kuwaondoa viongozi madhwâlim)."** Imepokewa na Ibn Shâhîn katika *al-Kitâb ul-Latwîf* Uk.15 yenye silsila ya upokezi iliyo swahîh. Abul Fadhl as-Saksakî al-Hanbalî (aliyekufa 683 AH) alisema kwenye kitabu chake, *al-Burhân fiy 'Aqâ'id Ahlil-Adyân;* Uk.96:

> **"Pote linalojulikana kwa jina la Mansûriyyah, ambalo ni wazushi wapotofu, waliwabandika jina Ahl us-Sunnah la Irjâ', si kwa sababu yoyote isipokuwa kwa**

amekosea katika mambo fulani, basi haki inatosha, lakini wasende zaidi ya hapo, mtu na achukuwe yenye kudhihirika wazi kutokana na matamshi yake. Anasema Sheikh **“imân ni kukiri kwa moyo, kutamka kwa ulimi, kutenda kwa viungo”** na anasema yakwamba **“kitendo ni miongoni mwa sehemu ya imân”** na anakufurisha kutokana na matamshi na kitendo na anasema yakwamba **“imân inazidi na kupungua”** na anamruhusu mja kusema **“mimi ni Mu’min insha-Allâh”**[4] – yote haya yanatokamana na

---

> **kutokana na Ahlus Sunnah kutowakufurisha watu wasioswali ikiwa hawakatai (uwajibikaji wake) wakidai yakwamba jambo hili (la kujiepusha kuwatangazia ukafiri) “linapelekea kuwa na Imân yakwamba Imân ni maneno peke yake na wala sio vitendo”.**

Hapa, maneno ya Sheikh Mash-hur yanahitaji kuzingatiwa kuhusu mfano wa mtu mmoja mjinga aitwae Salmân ‘Awân [“Abu Bakr bin Nâsir”], mwanafunzi wa ki-Marekani kwenye mojawapo ya Vyuo Vikuu nchini Saudi Arabia, ambaye aliyejitweka jukumu la maangamivu juu yake na kujaribu “kuwakosoa” ma-‘Ulamaa’ kutoka nyumbani kwake huko Texas, Marekani!? ‘Awân, ambaye aliyejaribu kujikongojea kuficha utambulisho wake halisi kwenye majukwaa ya mtandao kutokana na hofu kubwa ya kujitambulisha, amekuwa ni mwenye kueneza itikadi ya madai yakwamba Imâm al-Albâni na wanafunzi wake wametumbukia kwenye Irjâ’.

Kwa zaidi kuhusiana na mas’ala haya, angalia kitabu cha Sheikh Khâlid al-Anbarî, *Murji’ah wa Zama*, kimefasiriwa na Abu Hayyân Salal bin ‘Abdul-Ghafûr:
http://www.salafimanhaj.com/pdf/TheMurjiahOfTheEra_ebook,pdf

[4] **NUKTA YA MFASIRI:** Kulingana na Ahlus Sunnah inaruhusiwa kufanya *Istithnâ’* katika Îmân, ambayo ni mtu kuachana na kujiepusha nafsi yako kutokamana na kuwa na Îmân iliyo kamilika, kama vile kusema “Mimi ni Mu’mini, *Inshâ’allâh* (Akipenda Allâh)” au “Natumai yakwamba mimi ni Mu’mini”

Ibn Battah al-‘Ukbari, ametaja katika *al-Ibânah* (vol.2; Uk.872):

> **Kwahivyo hii ni njia ya waumini, na njia ya walio waerevu miongoni mwa Wanavyuoni, kushikamana na Istithnâ’, kuwa na khofu na matumaini. Wao hawaijui hali yao mbele ya Allâh! Na hawajui kuhusu vitendo vyao, ikiwa watatakabaliwa au kukataliwa!**

Vilevile amesema Ibn Battah:

> **“Kwa haya, njia ya Waislamu imeshapita na hivi ndivyo jinsi tabia zao za kawaida zilivyodumu, wale waliokuja waliyachukuwa kutoka kwa wale waliokuwa kabla yao. Hapana yoyote mwenye kupinga istithnâ’ hii katika Îmân isipokuwa Murji’ mchafu aliyepotoka ambaye moyo wake uliodanganywa na Sheitwân.”**

Imâm ‘Abdur-Rahmân bin MahdÎ amesema:

> **“Msingi wa Irjâ’ ni kuwachana na istithnâ’ (*yaani* kuachana na kujiepusha nafsi yako kutokamana na kuwa na Îmân iliyo kamilika).** Angalia katika *As-Sunnah* (1061) cha Imâm al-khalâl

Usûl wa Ahlus Sunnah katika imân na yoyote mwenye kuamini haya anakuwa sawa na hana hatia ya irjâ'. Lakini hatahivyo, baada ya haya katika baadhi ya mas'ala ya ki-Fiqhi, mimi naweza kusema jambo la ukweli kwa ulimi wangu, nalo ni kwamba "madh-hab yangu katika suala hili ni kadhaa na kadhaa" na kisha ukalichukuwa hilo na ukalipotosha msingi wa asili yake, kisha ukanukuu ki-makosa niliyosema mimi! Hii kweli ndiyo 'ilmu?! *Hii ni hasad! Hii ni hasad!*

Na kwa masikitiko sisi twajua kuhusu mas'ala, na huu ni ukweli ulio uchungu, twawajua baadhi ya watu, tulio na tajriba nao, kwa kuwatahini na kuwachunguza, na sisi ni wakweli na waaminifu katika ushahidi wetu na ma-'Ulamaa wengine kutoka sehemu nyengine za ulimwengu hawana budi wayajue haya – sisi tumewaona baadhi ya watu wanaochukuwa *fatâwâ* za wanavyuoni wa Hijâz, sio kutokana na mafungamano ya mapenzi kwao, bali ni kutokana na chuki zao juu ya Sheikh wetu![5] Sio hilo peke yake, baadhi yao wanawakufurisha ma-'Ulamaa' wa Hijâz, na hao ndiwo wale wale ambao wenye kuzungumza kumuhusu ndugu yetu, Sheikh 'Ali (*hafidhwahullâh*), na wakatumia kama dalili *fatâwâ* za watu wa Hijâz, na hapo hapo wao wanawakufurisha watu wa Hijâz!!? Sisi twawajua baadhi ya watu wasioswali katika *Haramayn*, Mjini Makkah na Madinah, wao wanawakufurisha ma-Imâm wa *Haramayn*, na ifikapo wakati wa kumzungumza Sheikh 'Ali, wao husema **"Mashekhe wa Hijâz na Baraza zima wametoa hukumu yakwamba amepotoka."** Wewe tangu hapo unawakufurisha hao (Mashekhe wa Hijâz)! Wewe unatumia matamshi ya "kuffâr" (kama usemavyo) kuwa ni dalili?! Huku ni kufuata *hawâ'* na fatwâ hii imefungua mlango wa kwenye shari kwa mwanafunzi wa ki-ilimu[6], ndugu yetu, Sheikh 'Ali, ni mwanafunzi wa ma-'Ulamaa' wakubwa, sasa ni somo gani lililotegemezwa juu ya utafiti huu wote uliofanywa? Ema ni kwamba fatwâ ilikuwa ni jambo lenye kusababisha *qeel wa qaal* na nukuu za makosa au mfano wake, na *wallâhi,* mfano wa fatâwâ kama hizi zimesababisha shari kubwa kwa Umma mzima. *Lâ hawla walâ quwwata illâ billâh!*

[5] **NUKTA YA MFASIRI:** Katika nchi za Magharibi, hata sisi tunaweza kusema yakwamba mambo kama hayo yameonekana, na hao viumbe waharibifu waliosherehekea na kufurahi wakati baadhi za fatâwâ zilipotolewa ki-makosa, na isitoshe, watu sampuli hiyo ni wale wenye kuwakufurisha viongozi watawala wa Saudi Arabia!?

[6] Imâm Ibn 'Uthaymin (*rahimahullâh*) pia alithibitisha haya.